Jibu: Ndio. Inawezekana kuuza bidhaa zilizokwishalipiwa kodi na Ushuru katika nchi yoyoyte mwanachama zaidi ya nchi ambayo bidhaa imetarajiwa kwenda. Hata hivyo, mwingizaji bidhaa anatakiwa awajulishe makamishna kuhusu nchi inayoingiza na zilikokuwa zinakwenda bidhaa, kulipa kodi katika nchi zinakouzwa na kudai marejesho katika nchi zilikokuwa zinakwenda bidhaa ambako kodi ililipwa awali.

**Swali: Je uondoshaji wa bidhaa utaendelea kufanyika katika mipaka ya ndani ya nchi wanachama?**

Jibu: Ndio. Kwa mizigo inayoondoshwa pale inapoingia kwa mara ya kwanza, ukaguzi utapunguzwa katika vituo vya mipaka ya ndani.

**Swali. Je bidhaa zinazozalishwa ndani ya jumuiya zitachukuliwaje?**

Jibu: Bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi hazilipiwi Ushuru pale zinaposafirishwa kwenda nchi nyingine ambayo ni mwanachama kama zinakidhi vigezo vya vya kanuni za uasili za jumuiya ya Afrika Mashariki. Hata hivyo bidhaa hizo zitatozwa kodi za ndani ambazo ni lazima zilipwe kabla bidhaa hazijasafirishwa kutoka nchi moja hadi kwenda nchi mwanachama zinakokwenda.

**Swali:Je mfumo wa kielektroniki wa kudhibiti mizigo, Electronic Cargo Tracking System (ECTC) hauna gharama zozote? na kama zipo ni nani anatakiwa alipe gharama hizo?**

Jibu: Una gharama. Gharama hizo zinalipwa na msafirishaji wa bidhaa.

**Swali: Ni vipi himaya Moja ya Forodha inaweza kutatua matatizo ya uingi wa vituo vya mizani?**

Jibu: Nchi wanachama wana dhamira ya dhati ya kupunguza idadi ya vituo vya upimaji mizigo kwenye mizani.

**Swali: Je ni vipi Mamlaka za Mapato zitahakikisha kuwa mtandao uliopo ni wa uhakika?**

Jibu: Majaribio yote yatafanywa kuhakikisha mtandao ni wa uhakika kabla ya kuanza kutumika.

**Swali:Ni nini kitatokea endapo mtandao utasumbua?**

Jibu: Njia mbadala zitakuwepo ili kuhakikisha shughuli zinaendelea.

**Swali:Ni nani atakuwa muhusika kama mizigo yenye dhamana haikufika mahali inapotakiwa ifike?**

Jibu: Wakala wa Forodha, msafirishaji wa bidhaa pamoja na muingizaji ndio watakuwa wahusika wakuu endapo mzigo utakiuka taratibu.

**Swali: Je wakala wengine wa serikali wanahusika vipi katika uondoshaji bidhaa katika kutimiza majukumu yao katika Himaya Moja ya Forodha?**

Jibu: Baadhi ya mawakala wa serikali wanaweza kuwaweka wafanyakazi wao katika sehemu ambazo bidhaa zinaingia kwa mara ya kwanza.

**Swali: Nani ana jukumu la kulinda mizigo inaposafirishwa?**

Jibu: Wakati nchi mwanachama itatoa ulinzi, wajibu wa ulinzi wa bidhaa ni wa wakala wa Forodha, msafirishaji na mwenye mzigo.

**Swali: Je,unafikiria kwamba kunaweza kuwa na upotezaji wa kazi?**

Jibu: Himaya Moja ya Forodha inatoa wigo mpana zaidi wa soko la ajira.

**Swali:Wakala wa usafirishaji (Shipping Line) anaweza kuchelewa kutoa orodha ya mizigo (Manifesti), nani ana jukumu la kulipa gharama zinazoongezeka?**

Jibu: Taratibu bora za kimataifa za utoaji orodha ya mizigo (Manifesti) kabla ya kuwasili kwa chombo cha usafiri tayari zinatumika kati ya wasafirishaji na mamlaka za bandari.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**


Ofisi ya TRA iliyo karibu nawe AU
Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi,
Mamlaka ya Mapato Tanzania
P.O.Box 11491, Dar es Salaam
Simu Na: 255-22-2119343/2119591-4
Nukushi: +255-22-2128593
Barua pepe: info@tra.go.tz
Tovutu: www.tra.go.tz

Kituo cha Huduma:
0800110016 (TTCL na Vodacom)
0786 800000 (Airtel)
0713 800333 ( Tigo )






# Maswali yanayoulizwa mara kwa mara juu ya Himaya Moja ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

**Maswali yanayoulizwa mara kwa mara juu ya Himaya Moja ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.**

**Swali: Himaya Moja ya Forodha maana yake ni nini?**

**Jibu:** Himaya Moja ya Forodha ni hatua ya kufikia umoja kamili wa Forodha unaofikiwa kwa kuondoa vikwazo vya kibiashara ikiwemo kupunguza udhibiti kwenye mipaka ya ndani.

**Swali: Himaya Moja ya Forodha ( SCT) inahusika na nini?**

Jibu:Inahusika na kuwezesha mzunguko wa bidhaa ndani ya mipaka bila vikwazo vyovyote ili kupunguza gharama za ufanyaji biashara.

**Swali: Himaya Moja ya Forodha (SCT) ina sifa gani?**

Jibu: Zifuatazo ni sifa za **Himaya Moja ya Forodha** (SCT)

- Bidhaa zinaondoshwa katika sehemu ya kwanza ya kuingilia kwenye himaya.
- Tamko juu ya Forodha linatolewa mara moja tu katika nchi bidhaa inapokwenda.
- Ushuru unalipiwa mahali ambapo bidhaa zinakwenda wakati bidhaa hizi zikiwa bado kwenye sehemu ya kwanza wa kuingilia.
- Bidhaa zinasafirishwa kwa dhamana moja kutoka bandarini hadi mahali zinapokwenda.
- Bidhaa zinasimamiwa na mfumo wa kielektroniki wa udhibiti mizigo, Electronic Cargo Tracking System (ECTS).
- Mifumo ya forodha yenye muunganiko
- Upunguaji wa usimamizi na ukaguzi wa ndani.

**Swali: Himaya Moja ya Forodha itaanza kutekelezwa lini?**

**Jibu:** Himaya Moja ya Forodha ilianzishwa Januari 1, 2014 kama majaribio katika ukanda wa kaskazini. Kwa ukanda wa kati, majaribio yataanza Aprili 2014 na baadaye kuanza kutumiwa na wanachama wote wa jumuiya ya Afrika Mashariki July 1, 2014.

**Swali: Faida zinazotokana na Uwanda wa usawa wa Forodha ni zipi?**

**Jibu**

- Kupungua kwa gharama za ufanyaji biashara kwa kuondoa milolongo isiyokuwa ya lazima.
- Kupunguza gharama za uendeshaji na usimamizi.
- Kuongeza mzunguko wa bidhaa, rasilimali watu, huduma na mitaji ndani ya soko la pamoja bila gharama zozote.
- Kuongeza kiwango cha uwekezaji wa kigeni, wa ndani ya nchi na miongoni mwa nchi wanachama.
- Kuchochea biashara kwa bidhaa zinazozalishwa na wanachama hususani bidhaa za kilimo kutoka eneo lenye wingi kwenda eneo lenye upungufu.
- Inachochea uhusiano kati ya sekta binafsi na ile ya umma.
- Uundaji wa mfumo wa kuzuia biashara za magendo katika jumuiya.
- Upunguzaji wa hatari zinazoambatana na kukiuka taratibu kwa bidhaa zinazosafirishwa nje kupitia nchi wanachama.
- Kuunda mfumo madhubuti wa kusimamia mapato.

**Swali: Nani wahusika wa uwanda wa usawa wa Forodha?**

Jibu: Wanajumuiya wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao ni - Burundi, Kenya, Rwanda, Tanzania, Uganda.

**Swali: Je, ni kweli kwamba watu wote wanaohusika na uondoshaji wa bidhaa watahamia Mombasa na Dar es Salaam kama sehemu za kwanza za kuingilia mizigo?**

Jibu: Sio kweli. Watu wote wanaohusika na uondoshaji bidhaa wanaweza kuchagua kufanya kazi kwa kutumia wawakilishi au wanaweza kuhamia Mombasa au Dar es Salaam kama sehemu za kwanza za kuingilia mizigo.

**Swali: Je ni Mombasa na Dar es Salaam tu ndizo zinatumiwa kama sehemu za kuingizia bidhaa kwa mara ya kwanza?**

**Jibu**: Hapana.Vituo vyote vya biashara vinavyopokea bidhaa kutoka nje ya wanajumuiya vinahesabika kama sehemu za kuingizia bidhaa kwa mara ya kwanza hii ikiwa ni pamoja na viwanja vya ndege vya kimataifa.

**Swali: Uondoshaji wa bidhaa utafanyikaje?**

Jibu: Bidhaa zitaondoshwa kwa kutolewa tamko katika nchi zinakokwenda.

**Swali: Je wakala wa Forodha kutoka kwenye nchi zinapokwenda bidhaa anaweza kupata huduma kwenye vituo zinakoingia bidhaa kwa mara ya kwanza?**

Jibu: Ndio. Mifumo ya Forodha inatumia tovuti na imewekwa katika mifumo inayoruhusu upatikanaji na muunganiko kutoka mahali popote.

**Swali: Je inawezekana kutolea tamko bidhaa zinazosafirishwa (Transit) kwenda miongoni mwa nchi mwanachama?**

Jibu: Hapana. Tamko la bidhaa zinazosafirishwa litatolewa pindi tu bidhaa toka nchi ya nje na kusafirishwa kupitia nchi wanachama kwenda nchi nyingine nje ya jumuiya.

**Swali: Ushuru wa Forodha utalipiwa wapi?**

Jibu: Ushuru wa Forodha utalipwa katika nchi ambayo bidhaa zinakwenda.

**Swali: Je wakala wa Forodha anaruhusiwa kufanya kazi katika nchi yoyote mwanachama katika Himaya Moja ya Forodha?**

Jibu: Ndiyo. Wakala wa wa Forodha ambaye amepewa leseni katika nchi moja mwanachama ataruhusiwa kufanya kazi katika nchi zingine wanachama kwa utambuzi wa pamoja.

**Swali: Je wakala wa Forodha anaweza kupata na kutumia mifumo yote ya Forodha katika Himaya Moja ya Forodha?**

Jibu: Ndiyo. Wanaweza kupata na kutumia mifumo yote ya Forodha. Pia watafundishwa namna ya kuitumia.

**Swali: Je ni lazima kuwa na dhamana ya mizigo katika Himaya Moja ya Forodha?**

Jibu: Hakutakuwa na dhamana kwa bidhaa ambazo tayari zimeshalipiwa Ushuru pala katika nchi ziliyofikia. Dhamana itatumika kwa bidhaa ambazo ni kwa ajili ya utunzaji maghalani, zinazoingizwa kwa muda, zinazosafirishwa kwenda nje ya jumuiya na zenye msamaha wa ushuru.

**Swali: Je kama mzigo umechaguliwa kufanyiwa ukaguzi katika sehemu unapoingia kwa mara kwanza, nani atakuwa msimamizi wa bidhaa kwa niaba ya muingizaji?**

Jibu: Wawakilishi katika sehemu mzigo unapoingia kwa mara ya kwanza ndio watakaosimamia ukaguzi wa bidhaa hizo.

**Swali: Je inawezekana kuuza bidhaa kwa nchi mwanachama zaidi ya nchi ambayo bidhaa zimefikia baada ya kulipiwa kodi?**